



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI**



KOZI YA WATOA HUDUMA KWENYE MABASI

1.0 UTANGULIZI

Kutokana na malalamiko kutoka kwa abiria wanaosafiri kwa mabasi kuwa wahudumu wanaotoa huduma ndani ya magari ya abiria wamekuwa wakitoa huduma isiyo na viwango, pamoja na kuwepo kwa Kanuni za Uthibitishaji Madereva na Usajili wa wahudumu wa Vyombo vya Moto Kibiashara (The Land Transport Regulatory Authority, Certification of Commercial Vehicle Drivers and Registration of Crew; Regulations, 2020). Hivyo, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na wasafirishaji ikiwemo Vyama vya Wamiliki wa Mabasi ya masafa marefu na mijini (TABOA na DARCOBOA) na wadau wengine wa sekta ya usafirishaji nchini waliona umuhimu wa kutoa mafunzo na kusajiliwa kwa watoa huduma ndani ya mabasi. Chuo Cha Taifa Cha Usafirishaji ni mionganini mwa vyuo vilivyopewa jukumu la kufundisha wahudumu wanaotoa huduma ndani ya mabasi ya masafa marefu na mijini. Chuo kimeandaa nyenzo zote za kufundishia na kujifunzia na kimejipanga kutoa mafunzo kwa kanda mbalimbali hapa nchini kama ilivyoainishwa kwenye jedwali 1.4.

1.1 Vigezo vya ushiriki

- Mshiriki awe na elimu angalau ya darasa la saba na anayejua kusoma na kuandika.
- Mshiriki anatakiwa awe na cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha taifa (NIDA) au leseni au kitambulisho cha mpiga kura.

1.2 Malengo ya Mafunzo

Kufikia mwisho wa mafunzo haya, mshiriki anatakiwa aweze;

- Kuwasiliana kwa ufanisi.
- Kuzingatia matakwa ya Huduma kwa Mteja.
- Kutoa huduma kwa abiria na utunzaji wa mizigo kwa kuzingatia kanuni za usafirishaji.
- Kushughulikia malalamiko ya mteja.
- Kutoa huduma kwa tiketi mtandao.

1.3 Mada zitakazofundishwa

- Utamaduni wa Huduma kwa Mteja.
- Uhusiano baina ya Watu.
- Huduma kwa Abiria na Utunzaji wa Mizigo.
- Usafi na Usalama katika Usafiri.
- Mwitikio wa Dharura.
- Tiketi Mtandao.

1.4 Mpango wa Mafunzo

NA	TAREHE	KANDA	KITUO
1.	02-07 Septemba, 2024	Kanda ya Ziwa	Mwanza
2.	14-19 Oktoba, 2024	Kanda ya Kaskazini	Arusha
3.	07-12 Oktoba, 2024	Dar Es Salaam	NIT
4	04-09 Novemba, 2024	Kanda ya Mashariki	Morogoro

Zingatia: Mafunzo yatafanyika endapo idadi ya washiriki itafika 40 kwa darasa.

Tafadhal thiбитisha ushiriki wako kwa kulipia ada ya mafunzo wiki moja kabla ya mafunzo.

Kwa Mawasiliano zaidi, wasiliana na;

Patrick Makule
+255 715 750 100
patrick.makule@nit.ac.tz

Honest Msaki
+255 743 988 939
honester.msaki@nit.ac.tz

Juma Omari
+255 658 821 252
Juma.omari@nit.ac.tz

1.5 Ada ya Mafunzo

Kila mshiriki atalipa ada ya mafunzo kwa gharama ya shilingi laki mbili (**200,000/=**). Aidha, Gharama za Usafiri na Malazi zitagharamiwa na mshiriki mwenyewe

1.6 Ada ya usajili LATRA

Kila mshiriki atasajiliwa na LATRA kwa gharama ya shilingi elfu ishirini (20,000/=).